

Je mama mjamzito anaruhusiwa kufunga?

Je mama mjamzito anaruhusiwa kufunga?..Na je watoto wadogo wanaruhusiwa kufunga na kusali? Na je inawezekana kufunga siku 40 bila kula?..

Kabla ya kufahamu kama mama mjamzito anaruhusiwa kufunga au la!..Hebu jiulize swali lifuatalo..{Je! Mtu katika hali ya kawaida anaruhusiwa kufunga siku 40 bila kula wala kunywa?..Au inawezekana mtu kufunga siku 40 bila kula wala kunywa na asife?}

Kama jibu ni ndio! basi Mjamzito naye anaweza kufunga.

Bwana Yesu alifunga siku 40 mchana na usiku bila kula wala kunya na hakufa...Na Mjaribu ibilisi alipomjia na kumwambia ageuze jiwe kuwa mkate..alimjibu na kumwambia imendikwa ..”mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litaokalo katika kinywa cha Mungu”

Mathayo 4:1 “Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi.

2 Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa.

3 Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate.

4 Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu”

Kama imewezezana mtu kuishi siku 40 bila kula wala kunya na hajafa basi inawezezana mjamzito au mtu mwingine yeote yule kufunga bila kupatikana na madhara yoyote isipokuwa tu afunge kwa Imani na si kwa kutimiza wajibu fulani, au kulazimishwa...

Nimewahi kukutana na kumthibitisha mtu binafsi ambaye amemaliza siku 40, bila kunywa wala kunywa na hawajafa...na wapo wengi tu wengine wanaokwenda mfungo hata wa wiki 2, 3 hadi 4..bila kula wala kunywa na wanaishi vizuri tu...Shetani anachowadanganya watu wengi siku hizi ni kwamba “jambo la kufunga siku 40 kama Bwana Yesu siku

hizi halipo"...Huo ni uongo wa shetani..

Hivyo mwanamke mjamzito anaweza kufunga hata katika hiyo hali ya ujauzito na isimuathiri yeye wala mtoto..

Lakini afunge tu kwa Imani, na si kwa dini wala mazoea, wala kulazimishwa..kama atafunga kwa dini na mazoea au kwa kulazimishwa basi ni afadhali asifunge kwa maana atapata madhara...lakini akifunga kwa Imani, huku binafsi akijiweka katika imani, utakatifu na ukamilifu... anaweza kumaliza hata siku 40 na mtoto akazaliwa akiwa na afya yake kamili na baraka tele.

Na sio tu mama mjamzito anaruhusiwa kufunga bali hata watoto..Wengi hawawaruhusu watoto wao wafunge wakihofia kwamba watadhoofika..Huo pia ni uongo wa shetani..mtoto kama anasukumwa ndani yake kufunga, hapaswi kuzuiliwa kwasababu "Mtu hataishi kwa mkate tu bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu"...Na Neno lenyewe ndio hilo kwamba " mambo mengine hayawezekaniki isipokuwa kwa kufunga na kusali". Hivyo watoto wadogo wanaruhusiwa kufunga kama watu wazima.

Maran atha!

Je mama mjamzito anaruhusiwa kufunga?

Mada Nyinginezo:

MSIJISUMBUE KWA NENO LOLOTE.

Je! taratibu za kufunga ndoa [yaani harusi] ni agizo la Mungu au ni mapokeo tu ya kibinadamu?

SIKU ILE NA SAA ILE.

Adamu alikuwa na watoto wangapi?

Je mama mjamzito anaruhusiwa kufunga?

Rudi Nyumbani:

Share on:

WhatsApp